# HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI (MST). MBAROUK S. MBAROUK MAKAMU MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI, WAKATI WA KUFUNGA MAFUNZO YA WATENDAJI WA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA, JIMBO NA KATA, YALIYOFANYIKA MKOANI IRINGA TAREHE 24 JANUARI, 2026 HADI TAREHE 26 JANUARI, 2026

- **Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume;**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume;**
- **Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi;**
- **Mwenyekiti wa Mafunzo;**
- **Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa ya Ruvuma na Songwe;**
- **Wasimamizi wa Uchaguzi;**

- **Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na Kata;**
- **Maafisa Uchaguzi;**
- **Maafisa Ununuzi;**
- **Wahasibu;**
- **Watendaji wa Tume;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha mafunzo haya ya siku tatu salama.

Nachukua nafasi hii pia, kuwapongeza waandaaji na waratibu wa mafunzo haya kwa kazi kubwa waliyofanya kuhakikisha mafunzo yanafanyika katika mazingira rafiki na kwa utaratibu uliokusudiwa. Vilevile, niwapongeze wakufunzi wetu kwa jinsi walivyowasilisha mada zao kwa umahiri na weledi wa hali ya juu uliowawezesha washiriki kufuatilia mafunzo ipasavyo.

**Ndugu Washiriki;**

Pili, nitumie fursa hii kuwashukuru nyote kwa ushirikiano mliouonesha kipindi chote cha mafunzo hadi tumemaliza kwa mafanikio.

Nawapongeza sana kwa michango mliyotoa wakati wote wa majadiliano kwa lengo la kujengeana uwezo wa kutekeleza majukumu ya uchaguzi na kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza.

Maswali mliyouliza na ufafanuzi uliotolewa na wakufunzi pamoja na michango yenu, imetoa mwanga na uelewa wa pamoja wa namna shughuli za uchaguzi zinavyopaswa kufanyika kwa mujibu wa Katiba, sheria, kanuni na maelekezo ya Tume.

Aidha, napenda kuwaahidi kuwa, mapendekezo mliyotoa yamechukuliwa na yatafanyiwa kazi ili kuimarisha uwezo wetu katika kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

**Ndugu Washiriki;**

Kama ilivyoelezwa wakati wa ufunguzi wa mafunzo haya, shughuli zote za uchaguzi zinaongozwa na Katiba, sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume. Hivyo, kwa niaba ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,

natumia nafasi hii kuendelea kuwasisitiza kuhusu umuhimu wa kutenga sehemu ya muda wenu kusoma Katiba, sheria na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Tume ili yawaongoze katika kusimamia uchaguzi utakaokuwa huru na wa haki.

Mkikutana na changamoto zozote msisite kufanya mawasiliano na watendaji wa Tume.

**Ndugu Washiriki;**

Jukumu lililopo mbele yetu ni kubwa na muhimu, linahitaji umakini na kujitoa. Ni matazamio ya Tume kwamba, baada ya kupatiwa mafunzo haya, mtatekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na weledi mkizingatia ratiba ya utekelezaji ili kufanikisha uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga unaotarajiwa kufanyika tarehe 26 Februari, 2026.

Kuhusu ajira za kupata watendaji wa vituo, tunayo imani kuwa mtateua na kuajiri watendaji wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi hii muhimu, jambo hili limekuwa likisisitizwa tokea siku ya kwanza ya mafunzo kwa kuwa hao ndio watakaosimamia zoezi la kupiga kura na kuhesabu kura vituoni. Kazi ambayo inahitaji umahiri, umakini na weledi katika kuitekeleza.

Ni imani yetu kuwa mafunzo ya watendaji wa vituo yatafanyika kwa ufanisi na weledi katika tarehe zilizopangwa kwenye ratiba ya utekelezaji wa shughuli za uchaguzi. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo ili waweze kufahamu majukumu yao na kuyatekeleza ipasavyo wakati wa uchaguzi.

**Ndugu Washiriki;**

Nawaasa kubandika matangazo mbalimbali ya kisheria kuhusiana na uchaguzi pamoja na mabango mbali mbali yanayotakiwa kwa mujibu wa maelekezo.

Ikumbukwe kuwa, wapo wadau mbalimbali wa uchaguzi kama vile waangalizi wa uchaguzi wa ndani ya nchi ambao wanafuatilia uendeshwaji wa uchaguzi na kiwango cha uzingatiwaji wa sheria zinazohusiana na uchaguzi. Hivyo, tuhakikishe tunazingatia maelekezo yanayotolewa na Tume kila wakati.

**Ndugu Washiriki;**

Nihitimishe kwa kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu ya uchaguzi yaliyo mbele yetu.

Baada ya kusema haya, natamka kuwa mafunzo haya ya siku tatu ya waratibu wa uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na kata, maafisa uchaguzi, maafisa ununuzi na wahasibu, yamefungwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**